**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

**FUNGU 16**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI KUANZIA 2018/2019 HADI JUNI, 2022

**SEPTEMBA, 2022**

## YALIYOMO

YALIYOMO .......... i

ORODHA YA MAJEDWALI .......... iii

1.0 UTANGULIZI .......... 1

1.1. Dira .......... 1

1.2. Dhima .......... 1

1.3. Muundo wa Kiutawala .......... 1

1.3.1. Divisheni za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali .......... 2

1.3.2. Vitengo vya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali .......... 2

1.3.3. Ofisi za Mikoa za Mwanasheria Mkuu wa Serikali .......... 2

1.4. Majukumu ya Ofisi .......... 2

2.0 UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 HADI JUNI, 2022/2023 .......... 3

2.1. Utekelezaji wa Malengo ya Ofisi .......... 4

2.1.1. Kuboresha huduma za kisheria katika majadiliano na upekuzi wa mikataba, uandaaji wa miswada, urekebu, kutafasiri na utoaji wa ushauri wa Kisheria Kazi zilizofanyika katika Divisheni ya Uandishi wa Sheria .......... 4

2.1.1.1. Kuandaa Miswada ya Sheria .......... 4

2.1.1.2. Utayarishaji wa Sheria Ndogo .......... 5

2.1.1.3. Ufasiri sheria .......... 6

2.1.1.4. Urekebu wa Sheria .......... 7

2.1.1.5. Kuandaa Maazimio ya Bunge .......... 8

2.1.1.6. Upekuzi wa Mikataba kutoka Serikali Kuu, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za a na Serikali za Mitaa ............................................. 9
2.1.1.7. Mapitio ya Mikataba Mikubwa ................................................................. 10
2.1.1.8. Ushauri wa Kisheria kwa Serikali Kuu, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa .................................. 11
2.1.1.9. Majadiliano ya Mikataba ........................................................................ 12
2.1.1.10. Majadiliano ya kumaliza migogoro/mashauri nje ya Mahakama ................. 12
2.1.1.11. Kuandaa Miongozo ya Kuboresha Utendaji kazi wa Ofisi ............................ 12
2.1.1.12. Kukuza Ushirikiano baina ya Taasisi na Taasisi pamoja na ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ........................................................................................ 13
3.0 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI ................................................... 14
4.0 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ................................... 15
5.0 HITIMISHO ......................................................................................................... 15

## ORODHA YA MAJEDWALI


JEDWALI NA. 2: IDADI YA MISWADA ILIYOANDALIWA NA KUPITISHWA NA BUNGE KUANZIA 2018/2019 HADI JUNI, 2022 .................... 4

JEDWALI NA. 3: IDADI YA SHERIA NDOGO ZILIZOANDALIWA KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 HADI JUNI, 2022 .................... 6

JEDWALI NA. 4: IDADI YA SHERIA ZILIZO TAFSIRIWA KUANZIA 2018/19 HADI JUNI, 2022 .................... 6

JEDWALI NA. 5: SHERIA ZILIZOFANYIWA UREKEBU KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 HADI JUNI, 2022 .................... 7

JEDWALI NA. 6: MCHANGANUO WA MAAZIMIO KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 HADI JUNI, 2022 .................... 9

JEDWALI NA. 7: IDADI YA HATI ZA MAKUBALIANO NA MIKATABA ILIYOFANYIWA UPEKUZI KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 HADI JUNI, 2022 .............. 10

JEDWALI NA. 8: IDADI YA MIKATABA ILIYOFANYIWA UPEKUZI NA KUTHAMINISHWA KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 HADI JUNI, 2022 10

JEDWALI NA. 9: IDADI YA MAOMBI YA USHAURI WA KISHERIA YALIYOFANYIWA KAZI KUTOKA KWA WADAU KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 HADI JUNI, 2022 .................... 11

JEDWALI NA. 10: IDADI YA MIKUTANO NA VIKAO AMBAVYO OFISI ILISHIRIKI KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 HADI JUNI, 2022 .................... 14

## 1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzishwa chini ya Ibara ya 59(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Jukumu kubwa la Ofisi hii ni kuishauri Serikali katika masuala yote ya Kisheria ndani na nje ya nchi katika maeneo ya Uandishi wa Sheria, Urekebu wa Sheria, Ufasiri Sheria, Upekuzi na Uchambuzi wa Mikataba mbalimbali ya kiuwekezaji. Aidha, Ofisi hii inaiwakilisha Serikali kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala yote ya kisheria yenye maslahi kwa Taifa kama yalivyooneshwa katika Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kuainishwa katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268.

### 1.1. Dira

Dira **(Vision)** ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni, *"kuwa Taasisi yenye ufanisi, kitaaluma na kuaminika katika kutoa huduma bora za kisheria kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"* ***(To be an efficient, professional and reliable institution in provision of quality legal services to the Government of the United Republic of Tanzania).***

### 1.2. Dhima

Dhima **(Mission)** ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni "*kutoa huduma za Kisheria zenye ubora kwa njia ya kuandaa Sheria, Upekuzi na Majadiliano ya Mikataba pamoja na Ushauri wa Kisheria kwa Maendeleo ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa"* ***(To provide quality legal services through Legislative Drafting, Contracts, Treaties and Advisory Services for social, economic and political development).***

### 1.3. Muundo wa Kiutawala

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanyiwa marekebisho kwa Tangazo la Serikali **Na. 48** la Mwaka 2018. Muundo mpya wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

wa Serikali una jumla ya Divisheni tano (**5**), Vitengo sita (**6**) na Ofisi za Mikoa **26** kama ifuatavyo: -

### 1.3.1. Divisheni za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

(i) Divisheni ya Uandishi wa Sheria;
(ii) Divisheni ya Mikataba na Makubaliano;
(iii) Divisheni ya Uratibu na Huduma za ushauri;
(iv) Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu; na
(v) Divisheni ya Mipango.

### 1.3.2. Vitengo vya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

(i) Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti;
(ii) Kitengo cha Fedha na Uhasibu;
(iii) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;
(iv) Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi;
(v) Kitengo cha TEHAMA; na
(vi) Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

### 1.3.3. Ofisi za Mikoa za Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Muundo wa Ofisi unahitaji kuwepo kwa Ofisi katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina Ofisi katika mikoa tisa (9) ambayo ni **Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Kilimanjaro, Mtwara, Mwanza, Kagera, Tabora na Tanga**.

## 1.4. Majukumu ya Ofisi

Kwa mujibu wa Hati Idhini ya Rais kuhusu Maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tangazo la Serikali **Na. 48** la Mwaka 2018, Ofisi hii inatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuishauri Serikali juu ya masuala yote ya kisheria ikiwemo Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania ni sehemu ya Mkataba ama ina maslahi katika Mkataba huo;

(ii) Kutoa ushauri kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Taasisi za Serikali kuhusu mchakato wa utungwaji wa sheria na masuala mengine yahusuyo sheria;

(iii) Kutoa ushauri stahiki wa sheria zilizotungwa na Bunge, Sheria Ndogo na maazimio mbalimbali;

(iv) Kuandaa miswada ya sheria kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni;

(v) Kuandaa hati zote za kisheria na maazimio kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(vi) Kushauri na kudumisha uhusiano kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa lengo la kuleta ufanisi kuhusu suala lolote lililopo Mahakamani na katika Mabaraza;

(vii) Kupokea taarifa kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka kwa dhumuni la kuishauri Serikali, Bunge na Mahakama;

(viii) Kuwasimamia Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali wote walioko katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika kutekeleza majukumu yao ya kisheria;

(ix) Kushiriki katika kudhibiti nidhamu ya Mawakili wa Kujitegemea kupitia Kamati ya Maadili ya Mawakili (Advocates Committee); na

(x) Kutekeleza jukumu lolote linaloweza kuwa muhimu kwa utekelezaji ulio na ufanisi wa majukumu na mamlaka ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 HADI JUNI, 2022/2023

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliweza kutekeleza malengo yafuatayo: -

(i) Kuboresha huduma za kisheria katika majadiliano na upekuzi wa mikataba, uandaaji wa miswada, urekebu, kutafasiri na utoaji wa ushauri wa Kisheria;
(ii) Kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutoa huduma za kisheria kwa ufanisi;
(iii) Kuboresha uwezo wa kusimamia, uhamasishaji wa rasilimali na uwajibikaji;
(iv) Kuimarisha utoaji wa elimu kuhusu masuala ya kisheria kwa Umma;
(v) Kupunguza maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI na kutoa huduma (lishe) kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI; na
(vi) Kukuza na kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa.

## 2.1. Utekelezaji wa Malengo ya Ofisi

### 2.1.1. Kuboresha huduma za kisheria katika majadiliano na upekuzi wa mikataba, uandaaji wa miswada, urekebu, kutafasiri na utoaji wa ushauri wa Kisheria Kazi zilizofanyika katika Divisheni ya Uandishi wa Sheria

#### 2.1.1.1. Kuandaa Miswada ya Sheria

Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi 2021/2022, Ofisi kwa kushirikiana na wadau wa sekta mbalimbali, iliwezesha kuwasilisha Bungeni jumla ya miswada **44** ya Sheria. Miswada iliyoandaliwa katika kipindi husika inaonekana katika **Jedwali Na. 2.** ***(Pia Angalia Kiambatisho Na. 5*****).**

**Jedwali Na. 1: Idadi ya Miswada iliyoandaliwa na kuwasilishwa Bungeni kuanzia 2018/2019 hadi 2021/2022**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Miswaada iliyowasilishwa bungeni |
|---|---|
| 2018/2019 | 13 |
| 2019/2020 | 10 |
| 2020/2021 | 7 |
| 2021/2022 | 14 |
| **Jumla** | **44** |

Chanzo: Divisheni ya Uandishi wa Sheria

Aidha, kati ya miswada 44 iliyoandaliwa katika kipindi hicho, Miswada 13 ilikuwa kwa ajili ya kutunga Sheria Mpya na Miswada 31 ilikuwa kwa ajili ya kutunga Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Written Laws Miscellaneous Amendments Bills) (WLMA) na sheria nyingine za marekebisho. Kupitia Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zilizotungwa katika kipindi hicho jumla ya sheria **295** zilifanyiwa marekebisho ili kuendana na wakati na kuziwezesha kukidhi malengo yaliyokusudiwa. Idadi ya Sheria zilizorekebishwa kupitia Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali kwa kila Mwaka wa Fedha ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.1.**

**Jedwali Na. 2.1: Idadi ya Sheria zilizorekebishwa kupitia kuanzia 2018/2019 hadi 2021/2022**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Sheria zilizorekebishwa |
|---|---|
| 2018/2019 | 57 |
| 2019/2020 | 87 |
| 2020/2021 | 70 |
| 2021/2022 | 81 |
| **Jumla** | **295** |

### 2.1.1.2. Utayarishaji wa Sheria Ndogo

Sheria Ndogo ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa Sheria Kuu kwa maana ya kujibu mahitaji au maswali ya – kitu gani **(what)**, kwa nini **(why)**, wakati gani **(when)**, nani **(who)**, wapi **(where)**, na kwa utaratibu gani **(how)**. Mara nyingi Sheria Kuu inakuwa tayari imeshajibu baadhi ya maswali na kuyaacha yaliyobaki kwenye uwanda wa Sheria Ndogo. Katika kipindi cha 2018/2019 hadi Agosti, 2022, Jumla ya Sheria Ndogo **3,457** zimeandaliwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali au kutumika kama ilivyokusudiwa ***(Angalia Kiambatisho Na. 6).*** Sheria hizi zinajumuisha Kanuni, Amri, Hati, Notisi, Sheria Ndogo (By- Laws) na

Matamko ya Serikali. Aidha, Mchanganuo wa Sheria Ndogo zilizoandaliwa umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 3.**

**Jedwali Na. 2: Idadi ya Sheria Ndogo zilizoandaliwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi Juni, 2022**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Sheria |
|---|---|
| 2018/2019 | 494 |
| 2019/2020 | 1,028 |
| 2020/2021 | 1,084 |
| 2021/2022 | 851 |
| **Jumla** | **3,457** |

Chanzo: Divisheni ya Uandishi wa Sheria

### 2.1.1.3. Ufasiri sheria

Sheria huwa zinatungwa kwa ajili ya kutumiwa na wananchi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, Kijamii na kisiasa na hivyo ni muhimu kuwa katika lugha ambayo wanaifahamu. Sheria nyingi zimetungwa kwa lugha ya Kingereza ambazo zinamfanya mwananchi kutoweza kuzielewa kwa urahisi hadi apate mkalimani wa kumsaidia kutafsiri. Katika kipindi cha 2018/19 hadi Agosti, 2022, Jumla ya sheria **297** zilitafsiriwa kutoka Lugha ya Kiingereza kwenda Lugha ya Kiswahili ***(Angalia Kiambatisho Na. 7*****). Idadi ya** Sheria zilizotafsiriwa kuanzia Julai, 2018 hadi tarehe Agosti, 2022 inaonekana kwenye **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na. 3: Idadi ya Sheria zilizo tafsiriwa kuanzia 2018/19 hadi Juni, 2022**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Sheria zilizopangwa kutafsiriwa | Idadi ya Sheria zilizotafsiriwa |
|---|---|---|
| 2018/2019 | 20 | 58 |
| 2019/2020 | 20 | 60 |
| 2020/2021 | 20 | 105 |
| 2021/2022 | 80 | 74 |
| **Jumla** | **140** | **297** |

Chanzo: Divisheni ya Uandishi wa Sheria

Aidha, kufuatia Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwezi Februari, 2021 kuhusu lugha ya Sheria na Mahakama kuwa Kiswahili, Ofisi yetu kupitia Divisheni ya Uandishi wa Sheria imeendelea chini ya uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria kushiriki kikamilifu na kutoa mwongozo katika Mazoezi ya Tafsiri yanayoendelea katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali.

#### 2.1.1.4. Urekebu wa Sheria

Katika kipindi cha 2018/2019 hadi Agosti, 2022, Ofisi kwa kushirikiana na wadau wa sekta mbalimbali, imeendelea na zoezi la Urekebu wa Sheria Kuu zote ambapo hadi sasa Ofisi ipo katika hata za mwisho kukamilisha Urekebu wa Sheria Kuu zote 446. Mwenendo wa Zoezi la urekebu ni kama inavyonekana kwenye **Jedwali Na. 5.** ***(Pia Angalia Kiambatisho Na. 8*****).**

**Jedwali Na. 4: Sheria zilizofanyiwa Urekebu kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi Juni, 2022**

| Mwaka wa Fedha | Kazi iliyofanyika | Matokeo ya Kazi |
|---|---|---|
| 2018/2019 | Utambuzi wa sheria na marekebisho yake | Jumla ya Sheria Kuu 449 zilitambuliwa na marekebisho yake |
| 2019/2020 | Maandalizi Index na kuandaa nakala laini | Kukamilika kwa Index nan akala laini kwa sheria 141 |
| 2020/2021 | maandalizi ya nakala laini na kuingiza marekebisho | kukamilika kwa nakala laini na uingizaji wa marekebisho kwa sheria zote 449 |
| 2021/2022 | uhakiki na uhariri kwa sheria zote 446 zilizobainika kuwa hai | Uhakiki na uhariri unaendelea |

Chanzo: Divisheni ya Uandishi wa Sheria

Kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali, kwa sasa Ofisi inaendelea na zoezi la uhakiki na uhariri wa sheria zote 446. Zoezi hili linafanyika kwa kushirikisha kikamilifu wataalamu

kutoka Wizara na Taasisi zinazosimamia sheria husika. Hadi sasa jumla ya Wizara 16 zimekwisha shiriki ambapo jumla ya Sheria 176 zimekwisha hakikiwa na kukaririwa kikamilifu teyari kwa ajili ya kupelekwa kwa Mpiga Chapa. Aidha, zoezi hili linahusisha Wataalamu wengine wa nje ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wakiwemo Waandishi wa Sheria Wastaafu. Lengo la ushirikishwaji huu ni kuhakikisha kuwa sheria zitakazotoka zinakuwa na kiwango stahiki. Zoezi hili la uhakiki na uhariri linatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 15 Desemba, 2022. Baada ya hapo hatua za uchapaji zitafuata. Lengo ni kutoa toleo la urekebu wa Sheria Kuu zote ifikapo Januari, 2023.

**(i) Urekebu wa Sheria Ndogo**

Sambamba na Urekebu wa Sheria Kuu, Ofisi imeanza maandalizi ya Urekebu wa Sheria Ndogo. Zoezi hili linahusisha Sheria Ndogo zote zilizokuwepo hadi wakati wa zoezi la mwisho la Urekebu la mwaka 2002 na Sheria Ndogo zote zilizotungwa baada ya hapo. Divisheni imekamilisha utambuzi wa Sheria Ndogo zote zilizotungwa kuanzia mwaka 1920 mpaka Juni 2021. Utambuzi huu umebaini kuwepo kwa jumla ya Sheria Ndogo 40,105. Aidha, kwa sasa Divisheni inaendelea na maandalizi ya "Index" itakayoongoza zoezi la Urekebu wa Sheria Ndogo.

**2.1.1.5. Kuandaa Maazimio ya Bunge**

Uaandaaji wa Maazimio ya Bunge kwa ajili ya kuridhia mikataba na itifaki za Kimataifa kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja ya majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Agosti, 2022, Maazimio **20** ya kuridhia Itifaki na Mikataba mbalimbali yaliandaliwa na kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa (**ratification**). Mchanganuo wa maazimio hayo ni kama yanavyoonekana katika **Jedwali Na. 6.**

**Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa maazimio kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi Juni, 2022**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Maazimio yaliyopitishwa na Bunge |
|---|---|
| 2018/2019 | 3 |
| 2019/2020 | 12 |
| 2020/2021 | 2 |
| 2021/2022 | 3 |
| **Jumla** | **20** |

Chanzo: Divisheni ya Uandishi wa Sheria

### 2.1.1.6. Upekuzi wa Mikataba kutoka Serikali Kuu, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za a na Serikali za Mitaa

Lengo la Ofisi ni kushiriki katika majadiliano ya Mikataba Mikubwa ya Kitaifa na Kimataifa na kufanya upekuzi wa Mikataba yote ya Kitaifa na Kimataifa inayoihusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi tarehe Agosti, 2022, Jumla ya Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa **4,957** ilifanyiwa upekuzi na Hati za Makubaliano (**Memorandum of Understandings - MoUs**) **431** zilifanyiwa upekuzi **(Angalia Jedwali Na. 7)**. Kati ya mikataba **4,957** iliyofanyiwa upekuzi, mikataba **2,314** iliyothaminishwa katika sarafu mbalimbali, Mikataba **1,797** ilikuwa na thamani ya **Shilingi za Kitanzania trilioni 135.78,** Mikataba **390** ilikuwa na thamani ya **Dola za Marekani 265,845,571,963.92** sawa na **Shilingi za Kitanzania trilioni 613.84** na Mikataba **127** ilikuwa na thamani ya fedha ya **Jumuiya ya Ulaya (Euro) 17,524,441,374.318** sawa na **Shilingi za Kitanzania trilioni 45.06 (Angalia Jedwali Na. 8).** Mikataba hiyo ilihusisha masuala ya manunuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo, utoaji wa huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na Barabara.

**Jedwali Na. 6: Idadi ya Hati za Makubaliano na Mikataba iliyofanyiwa upekuzi kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi Juni, 2022**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Hati za Makubaliano | Idadi ya Mikataba |
|---|---|---|
| 2018/2019 | 98 | 1,230 |
| 2019/2020 | 124 | 1,031 |
| 2020/2021 | 39 | 1,085 |
| 2021/2022 | 170 | 1,611 |
| **Jumla** | **431** | **4,957** |

Chanzo: Divisheni ya Mikataba

**Jedwali Na. 7: Idadi ya Mikataba iliyofanyiwa upekuzi na kuthaminishwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi Juni, 2022**

| Mwaka wa Fedha | Mikataba iliyokuwa katika Fedha za Kitanzania | | Mikataba iliyokuwa katika Dola za Marekani | | Mikataba iliyokuwa katika Fedha ya Jumuiya ya Ulaya | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya Mikataba | TZS (000,000) | Idadi ya Mikataba | Dola ($) | Idadi ya Mikataba | Euro(€) |
| 2018/2019 | 523 | 3,472,971.20 | 93 | 3,732,120,495.93 | 33 | 1,314,629,084.84 |
| 2019/2020 | 365 | 6,343,360.38 | 91 | 257,218,953,239.05 | 34 | 373,353,677.15 |
| 2020/2021 | 382 | 5,784,759.57 | 97 | 1,592,343,071.01 | 30 | 15,425,439,764.35 |
| 2021/2022 | 527 | 120,170,286.09 | 109 | 3,302,155,157.93 | 30 | 411,018,847.98 |
| | 1797 | 135,771,377.24 | 390 | 265,845,571,963.92 | 127 | 17,524,441,374.32 |

Chanzo: Divisheni ya Mikataba

### 2.1.1.7. Mapitio ya Mikataba Mikubwa

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeunda vikosi kazi vinavyohusisha wataalamu kutoka Taasisi zinazohusika na Mikataba ya Utafutaji na Uzalishaji wa Gesi Asilia, Mafuta pamoja na Uzalishaji Umeme ili kufanya mapitio ya Mikataba hiyo kwa lengo la kubaini kama ina maslahi kwa Taifa. Aidha, kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi tarehe Juni, 2022 Ofisi imefanya mapitio ya Mikataba **13** ya Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi, Mikataba mingine takriban **70** inayohusu Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Songo Songo na Mikataba mingine **11** ya Wazalishaji Wadogo wa Umeme.

### 2.1.1.8. Ushauri wa Kisheria kwa Serikali Kuu, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Katika utekelelezaji wa Sera, Mipango na Sheria za nchi mara nyingi yanajitokeza maeneo ambayo yanahitaji ushauri wa kisheria ni kwa namna gani bora ya kuendana katika masuala mbalimbali yanayojitokeza au kabla ya utekelezaji. Ofisi ina jukumu la kutoa ushauri wa Kisheria kwa Serikali Kuu, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na wananchi kwa lengo la kuhakikisha Serikali na Taasisi zake zinapata faida kutokana na utekelezaji wa majukumu yake na hivyo kuikinga kutoingia katika madhara au kesi mbalimbali wakati wa utekelezaji wa majukumu hayo kwa kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu za nchi zinafuatwa. Katika kipindi cha kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi Juni, 2022 Ofisi ilipokea na kutoa ushauri wa kisheria kwa maombi **4,254**. Maombi hayo ni kutoka Serikali Kuu, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na wadau wengine. Ongezeko hili linatokana na kuanzishwa kwa Divisheni ya Uratibu na Huduma za ushauri inayoainishwa kwenye Maboresho ya Muundo wa Ofisi ulifanyiwa marekebisho kwa Tangazo la Serikali **Na. 48** la mwaka 2018 na kuanza kutumika Mwezi, Julai, 2018. Mchanganuo wa Wadau walioleta maombi upo kwenye **Jedwali Na. 9.**

**Jedwali Na. 8: Idadi ya Maombi ya Ushauri wa Kisheria yaliyofanyiwa kazi kutoka kwa wadau kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi Juni, 2022**

| Jina la Mdau | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Wizara | 84 | 380 | 393 | 327 | 1184 |
| Taasisi za Serikali | 24 | 243 | 254 | 324 | 845 |
| Mashirika ya Umma | 1 | 22 | 34 | 122 | 179 |
| Mamlaka za Serikali | 16 | 20 | 39 | 101 | 176 |
| Wakala wa Serikali | 3 | 19 | 28 | 82 | 132 |
| Mamlaka za | 8 | 57 | 65 | 68 | 198 |

| Jina la Mdau | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Serikali za Mitaa | | | | | |
| Makampuni | 19 | 78 | 83 | 76 | 256 |
| Wadau wengine/Watu binafsi | 19 | 310 | 267 | 688 | 1284 |
| **Jumla** | **174** | **1,129** | **1,163** | **1,788** | **4,254** |

Chanzo: Divisheni ya Uratibu na Ushauri wa Kisheria

#### 2.1.1.9. Majadiliano ya Mikataba

Ofisi inaendelea kushiriki katika majadiliano ya mikataba ya Miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Majadiliano ya Mradi wa Kubadilisha Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquified Natural Gas – LNG) na Mradi wa Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Bagamoyo (Bagamoyo Special Economic Zone project). Aidha, kwa usimamizi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Timu ya Serikali ya Majadiliano ilikamilisha majadiliano na kusaini Mkataba wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP). Aidha, ushiriki wa Serikali katika majadiliano hayo kunaiwezesha Serikali kushiriki moja kwa moja katika uandaaji na usimamizi wa miradi hasa inayotumia rasilimali za nchi kwa maendeleo ya Taifa.

#### 2.1.1.10. Majadiliano ya kumaliza migogoro/mashauri nje ya Mahakama

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea na majadiliano ya kumaliza migogoro ya mashauri mbalimbali nje ya Mahakama za Kimataifa, Mabaraza ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji na Biashara, Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahakama ya Rufani. Lengo kuu la kumaliza migogoro kwa njia ya majadiliano ni kupunguza gharama za fidia na uendeshaji wa mashauri kwa migogoro yenye hoja dhaifu kwa upande wa Serikali.

#### 2.1.1.11. Kuandaa Miongozo ya Kuboresha Utendaji kazi wa Ofisi

Jumla ya miongozo **10** iliandaliwa kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa majukumu ya Ofisi. Miongozo hiyo ni pamoja na: -

(i) *Draft Guidelines for Contract Termination;*
(ii) *Draft Guidelines for Vetting Procurement Contracts;*
(iii) *Draft Guidelines for Vetting Investment Contracts;*
(iv) *Draft Guidelines for Vetting Natural Wealth and Resources Contracts;*
(v) *Draft Guidelines for Vetting Treaties and International Agreements;*
(vi) *Draft Guidelines for Management of Contracts and Reporting of Suspicious Corrupt Activities on the Performance of Contracts;*
(vii) *Draft Guidelines for Negotiation of Contracts;*
(viii) *Draft Guidelines for Provision of Legal advice;*
(ix) *Draft Guidelines for Regional and District Legal* Advisory Committees; na
(x) *Draft Guideline for By-Laws making in the Local Government Authorities was developed*.

#### 2.1.1.12. Kukuza Ushirikiano baina ya Taasisi na Taasisi pamoja na ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

Lengo ni kuhakikisha Maslahi ya Taifa yanapewa kipaumbele katika mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwenye majadiliano mbalimbali ya mikataba inayosainiwa na Serikali.

Katika kipindi cha kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi Juni, 2022, Ofisi ilishiriki kikamilifu katika jumla ya Mikutano **1,431** ya majadiliano na vikao kazi mbalimbali vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kutoa maamuzi ya kisheria na kutetea maslahi mapana ya Taifa kwa ujumla. Mikutano hiyo inajumuisha mikutano ya Kitaifa, Jumuiya ya Afrika Mashariki **(EAC),** Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizopo Kusini mwa Afrika **(SADC),** Umoja wa Afrika **(AU),** na Umoja wa Mataifa **(UN)**. Mikutano hiyo ilihusu majadiliano ya mikataba ya kibiashara na

mikataba ya mahusiano ya Kikanda na Kimataifa na mikutano ya Kamati mbalimbali za uanachama wa Mamlaka mbalimbali zinazohusika na majadiliano ya mikataba. Mchanganuo wa Mikutano umeonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 10.**

**Jedwali Na. 9: Idadi ya Mikutano na Vikao ambavyo Ofisi ilishiriki kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi Juni, 2022**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Mikutano | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | National | EAC | SADC | AU | UN | |
| 2018/2019 | 40 | 9 | 3 | | | **52** |
| 2019/2020 | 476 | 13 | 5 | 2 | 3 | **499** |
| 2020/2021 | 293 | 4 | 3 | 2 | | **302** |
| 2021/2022 | 528 | 31 | 15 | | 4 | **578** |
| **Jumla** | **1,337** | **57** | **26** | **4** | **7** | **1,431** |

## 3.0 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI

Katika kutekeleza majukumu kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Juni, 2022 Ofisi ilikumbana na changamoto zifuatazo:

(i) Kuongezeka kwa wigo wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali usiowiana na rasilimali fedha na watu zilizopo. Ongezeko hilo linatokana na maelekezo ya Serikali na ya Chama Tawala ya kusogeza na upatikanaji wa huduma za ushauri wa kisheria kwa wananchi;

(ii) Kushindwa kutekeleza majukumu muhimu ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa kutokana na uwezo mdogo wa kifedha kunakosababisha ushiriki mdogo katika shughuli za kikanda na kimataifa;

(iii) Kuwepo kwa miundombinu duni ya TEHAMA ambayo inasababisha upatikaji wa taarifa mbalimbali za kiutendaji wa Ofisi kuwa mgumu na kuwanyima wananchi haki ya kujua masuala yanayoendelea katika sekta ya Sheria. Baadhi ya taarifa hizo ni Sheria mpya zilizopitishwa na Bunge, Sheria zilizofanyiwa marekebisho, Sheria zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, Mikataba mbalimbali iliyoridhiwa na nchi yenye maslahi kwa Taifa;

(iv) Ofisi kuwa na upungufu wa vitendea kazi kama magari, samani, kompyuta, mashine za kudurufu na vitabu vya sheria ambavyo husababisha ofisi kutotekeleza majukumu yake kwa wataki;

(v) Kutofanyika kwa mafunzo ya mara kwa mara hususan katika maeneo ya upekuzi wa mikataba, uratibu na utoaji ushauri wa kisheria, uandishi wa sheria, urekebu, na tafsiri sheria;

(vi) Watumishi wabobezi kuacha kazi au kuhamia taasisi zenye maslahi mazuri zaidi;

(vii) Gharama ya kukodi majengo kwa ajili ya ofisi katika mikoa yote 26 ni kubwa; na

(viii) Ofisi kushindwa kuendana na kasi ya ongezeko la watumiaji wa Sheria mbalimbali hususan matumizi ya sheria zilizo tafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili na Sheria zilizofanyiwa urekebu ili ziendane na wakati.

## 4.0 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa hapo juu, Ofisi inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

(i) Kuhakikisha sheria zinaandikwa kwa wakati na kwa weledi kwa ajili ya kupata matokeo yaliyo chanya hasa kwa maendeleo ya wananchi;

(ii) Kufanya urekebu wa Sheria mbalimbali kwa wakati na mara tu zinapofanyiwa marekebisho na Bunge ili ziendane na wakati;

(iii) Kufanya upekuzi wa Mikataba kwa wakati ili kuhakikisha kuwa Mikataba yote inayoingiwa na Serikali inakuwa na maslahi mapana kwa Taifa. Kwa Mikataba iliyokwishasainiwa, Ofisi itaendelea kuifanyia mapitio kwa kushirikiana na Taasisi nyingine;

(iv) Kuendelea kusimamia maadili ya watumishi wote wa Ofisi ili kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria na miongozo ya taaluma yao na maadili kwa ujumla.

(v) Kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi ili kuleta motisha kwa watumishi na kuongeza ari na ufanisi wa utendaji kazi;

(vi) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo wa Miaka Mitatu (2020/21 – 2022/23); na

(vii) Kuendelea kuimarisha mfumo wa kieletroniki na miundombinu yake kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Ofisi.

## 5.0 HITIMISHO

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama taasisi muhimu katika kutekeleza azma ya Serikali ya kufikia uchumi wa viwanda, itaendelea kuhakikisha inatoa huduma za kisheria kwa ufanisi kwa serikali, taasisi zake na wananchi kwa ujumla kwa kuzingatia kwamba, utekelezaji wa majukumu ya ofisi unachangia kufikiwa kwa malengo ya ukuaji wa sekta nyingine na uchumi wa nchi kwa ujumla hususan katika eneo la usimamizi wa

mikataba, utungaji wa sheria, urekebu wa sheria, ufasiri wa sheria na kutoa ushauri wa kisheria.